

WTE: Elimu na Wajibu kwa Jamii

Imeandikwa na Logan Cochrane

mchangiaji: William Chu Kwan

Kama mwanafunzi na mkaaji wa kambi la wakimbizi la Lugufu, Edward amechukua jukumu la kiongozi wa jamii kwa kuwaelimisha viongozi 33 wa vijiji vingine kuhusu HIV/AIDS. Edward ni mmoja kati ya waliyochaguliwa kushiriki kwa semina kuhusu HIV/AIDS na atachangia kwa kuwaelimisha wengine. Mbinu hii itadhamini kuwa habari halali na sahihi zitafikia watu wote. Habari hizi zitawafikia wafanyakazi wanaohusika na makanisa, shule, mikataba , na semina zingine.

Katika miradi yote ya WTE kuna hamu ya kupatia mamlaka za mitaa uwezo wa kujitegemea. Katika awamu ya mipango, mamlaka za mitaa zilikarabati na kubuni mipango itakayoweza kutekelezwa kwa urahisi katika mitaa yao. Katika awamu ya utekelezaji, mamlaka za mitaa ziisimamia mipango na kuwajibika katika sekta ya fedha.

Mmoja ya mashirika yetu ni ACDA (Shirika la Maendeleo la Agoro). Kama ilivyo na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali, wakurugenzi wa ACDA ni wakujitolea. Uhaba huu wa fedha unapatikana katika mashirika mengi yanayohusika na WTE. Mashirika haya yalibuniwa kwa kutilia hali mahitaji ya jamii. Hapo awali, ACDA ilibuniwa kama shirika la kukusanya pesa za koukoa miili ya watu waliouliwa na LRA (Jeshi la Upinzani la Lord) na kuwapatia mazishi ya hadhi. Kufanya kazi katika eneo lililoharibiwa na vita hakujaua mioyo ya watu 78 waliojitolea. Hivi karibuni, ACDA ilibuni kituo cha watoto kwa usaidizi wa Shirika la Mataifa. Kituo hiki cha watoto kinabuwezo wa kuwasajili watoto 1400, na kina shule ya ufundi na teknolojia ya habari, kwa fadhili ya michango kutoka kwa shirika la kimataifa, RESPECT.

Licha ya mipango kabambe ya ACDA ya siku za usoni, shirika hili hukosa fedha na mbinu za kuitekeleza mipango hii. WTE hushirikiana na ACDA kutekeleza mipango. Mmoja ya mipango hii ni kuelimisha watu kuhusu HIV/AIDS. Semina na vifaa vya elimu hazidhamini kuwa shirika hili linaeza kujitegemea. Hivyo basi, mtu mmoja katika jamii huchaguliwa kuelimisha na kutoa msaada kila wakati. Mjumbe huyu hudhibiti upanuzi wa kituo hiki. Mapanuzi tele hufanyika wakati kituo cha elimu kimebuniwa. Hivi ndivyo jamii itaweza kujitegemea, na sio lazima itegemee mashirika ya kigeni. Pia, mipango hii husababisha hisia za ujamii ni umoja. Lengo la mwisho la WTE ni kuleta mabadiliko na kuleta adhari za kudumu katika jamii.